MAANA HALISI

YA

IMAAN

(I)

AL FAQEER AHMAD SHEIKH,
DIBAJI: AL HABIB SEYYID UMAR
BIN ABDALLAH (MWINYIBARAKA),
MAJAALIS EL ULAA EL QADIRIYYA,
DAR ES SALAAM TANZANIA.

YALIYOMO

1. Shairi Mwenyezi Dawamu (Sheikh Ally mzee)……ii

2. Dibaji: (Sayyid Omar Bin Abdallah Mwinyi Baraka)..iv

3. Shukrani…….....vii

4. Utangulizi…….……...ix

5. Imaan Khatua ya Kwanza…….……1

6. Imaan Khatua ya Pili…….…….…..12

7. Imaan Khatua ya Tatu……...…....15

8. Ngome Ya Kwanza "Yaqin"…….……...18

9. Ngome Ya Pili "Ikhlaas"……..…20

10. Ngome Ya Tatu "Kutekeleza Faradhi"…….…….....23

11. Ngome ya Nne "Kuacha yaliyoharamishwa".....……...26

…

12. Ngome ya Tano "Kutekeleza wajibati"…….. ...28

13. Ngome ya Sita "Kutekeleza Sunna"…….....…..29

14. Ngome ya saba "Adabu"……...……...31

MWENYEZI DAWAMU:

Kwa jina lako Jahali, nalo ninalokadimu.
Tukufu na la awali, Rahmani na Rahimu.
Shabihi wala mithali, hana mfano adhimu
Mwenye Enzi ya Dawamu, katukuka Maulaya.

Uliyoumba arishi kubwa iliyo adhimu,
Kursiyu na Firashi, na Lawhi na kalamu.
Matukufu hayaeshi, Fi-Shani kulla yomu.
Mwenye Enzi Dawamu, katukuka Maulaya.

Kauni na vilivyomo, toka Alifu na Mimu.
Jumla na waliyomo, katika kila Isimu.
Kisicho na kilichomo, ni vyote vyako Halimu.
Mwenye Enzi Dawamu katukuka Maulaya

Ewe unao Sabihiwa, na kila kitu Dawamu.
Pia na kuhimidiwa, na vitu vyote Ayamu.
Kattu usiawe na malaika kiramu.
Mwenye Enzi Dawamu katukuka Maulaya.

Ndiwe unayefariji, daima unayekimu.
Kadhiya na hawaiji, zote hutatukirimu.
Bila ya wewe haiji, neema kila msimu.
Mwenye Enzi Dawamu Katukuka Mauyalaya

Penye haki Mola pako, tufutie maathiu.
Penginepo wajawako, hatupajui adimu.
Tumeeelekea kwako Molla wetu ya Alimu.
Mwenye Enzi Dawamu katukuka Maulaya

Tajiriba na fadhaa, kwa mja hilo lazimu.
Moyoni weka rajaa, kwa Mola ukizimu.
Usikatie tamaa Rabi atakukirimu.
Mwenye Enzi Dawamu Katukuka Maulaya

Kwashauku na vipaji, vikubwa vilo timu.
Vipi visitoe maji vidole vyake Hashimu.
Mola kampa faraji, mpenzi wake Karimu.
Swala watu wa salamu mpenzi wa Maulaya.

Zinaandama athari, kwa bwana mwenye ulumu
Alieacha dahari, nyoyoni mwa wanaadamu.
Jumla na Asrari, ziloondoa zidi hamu.
Swala watu wa Salamu, Mpenzi Maulaya.

Dhati ya nyoyoni mwetu, Mola anatufamu.
Juu ya Mtume wetu, mwenye Badru tamamu.
Kumpenda haki yetu, ilo kubwa Adhimu.
Swala watu wasalamu, Mpenzi Maulaya.

Rabi Sala zenye Huba, mfikizie Hashimu.
Kadhaali na sahaba, pia wote Maimamu.
Pasiwepo na hijabu, hapa mpaka kiyamu.
Ndie Shafii Anamu, Mpanzi wa Maulauya

DIBAJI

DIBAJI

DIBAJI

بسم الله والحمد لله والصلاة والسلام علي
خير خلق الله واله و صحبه ومن واما بعد

Kitabu hiki kilichoandikwa na mtoto wetu kimekusanya mengi yenye maana kubwa na ya msingi wa Kiislamu. Amejulisha umoja wa Mwenyezi Mungu na mapenzi yake juu ya Mtume Muhammad SAW Aya alizozitia katika kitabu hiki zinathibitisha kuwa yeye Sayyidna Muhammad ni mjumbe wa mwisho kabisa wa pekee ambaye hapana njia yoyote nyingine ya kumjua Mwenyenzi Mungu, ya kumtii na kujisogeza Kwake ila yeye Mustafa aliechaguliwa. Ahmad amefanya vizuri kutaja baadhi yaliolazim juu ya Mwislam na yalioharamishwa, na kuonyesha alama za kweli za Muumini, katambulisha umuhimu wa kutengeneza Moyo, kwani vitendo vya viwili wili, ijapokuwa Muislamu hana budi navyo havitoshi ikiwa moyo umeachiwa uwe mchafu. Moyo ukiwa msafi ndipo vitendo vitakapokubaliwa, hapana Shaka kuwa tabia njema ndio lengo la Dini ya Kiislam, na kitabu hiki kimeacha wazi hayo Alhasili atakaekisoma kwa Insafu na kuzingatia atapata faida nyingi zilohusu Islam, Imani na Ihsani. Mwenyezi Mungu ambariki aliyekitunga.

Omar Abdallah

SHUKRANI:

Namuhimidi Mnyezi Mungu na namtakiya wingi wa rehma Bwana Mtume Muhammad SAW. Na jamaa zake pamoja na sahaba zake watukufu waliokuwa na sifa nyingi za kuutukuza Uislamu siku zile ulivyokuwa mchanga na dhaifu bila chembe ya maendeleo, miaka elfu na arbaa mia leo.

Namshukuru Mnyezi Mungu kwa kuileta kwake Nuru (Ilmu na Bwana Mtume SWA) ambaye kwa kuwaka kwake muda wa miaka ishirini na nne kasoro moja kwa idadi ya:-

لااله الاالله محمد رسول الله

Ulimwengu mzima uliokua gizani umebaki mwenye mwanga hadi leo lau baada ya kuzima Nuru hiyo, siku ile ya jumatatu (Mfungo 6 AH 11) tarehe 8 Juni, mwaka 632 tangu kuzawa Nabii Isa As. Kwa rehma zake mwanga huo huo ukiwa umetufikia nasi kwa njia ile aliyoisema mwenyewe SAW:-

"wanazuoni wao ndiyo warithi wa mitume Aleyhi-Salam".

Wallahi nimejihisi kuwa na wajibu mkubwa kuwatolea shukrani Pamoja na kuwaombea Mnyezi Mungu Msamehevu awaghufurilie dhambi zao na kuwamiminia Neema na Rehma kubwa kwa ambao wamekufa na walio hai: Yaa Rab, Yaa Allah yote haya wayasikia, dua yangu hii nitakabaliya kwa jaha ya Mbora wa Manabiya Bwana Muhammad SAW. Khayrul Baryya – Aamin.

Miungoni mwao hao ulamaa, namshukuru Al habib Seyyid Omar Bin Abdallah (Mwinyi Baraka) kwa kupitia kwake na kukiandikia Dibaji kitabu hiki, pia shukrani zangu za dhati nazitoa kwa wafuatao :-

Sheikh Ally Mzee comorian wa Dar-es-Salaam pamoja na Habib - Swaleh (kwa kutunza kwao Nuskha zetu) na kumuonyesha Al Habib ili kuzisahihisha. Wafadhili wa mradi wenyewe:-

1. Salim Ahmed Bahashwan (Chairman of Yemen Comm (T).
2. Mohamed A. Ahmed Es- Hag (Scandinavia Bus Service Dar-es – Salaam)
3. Mohamed Mbaraka Salim (Timami Traders Zanzibar).
4. Ahmed Said Bamaga (Total Petrol station Mwenge Dar-es- Salaam)
5. Abdallah S. Abdallah (Shekha Pertol station Kibaha).
6. Al-Mahd (Almarhum) Dar-es-Salaam.
7. Jamal Ahmed (Pertol Station Kibaha).

8. Ndugu Ally Said wa Agip Dar-es- Salaam) na mwisho
Ahli-Majaals wote wa Dar-es-Salaam kwa kunipa moyo kwao ili kukichapisha kitabu hiki.

Al Faqeer Ahmad Sheikh,
DAR ES SALAAM.

UTANGULIZI:

بسم الله الر حمن الر حيم

Naanza safari yangu hii (Yaani kuandika kwangu juu ya Kuijuvya Imaan dhati yake ni nini, na ni vipi na ina maana gani si kwa Mwislam tu, bali kwa binadamu kwa jumla). Kwa kuomba muawana wa Mnyezi Mungu ili nisije nikatindikiwa na yote niliyoyakusudia, kwa kufuata kauli yake Bwana Mtume S.A.W:

كل ذي بال لايبدء فيه باسملة فهي اقطع اي القليل البركة

"Kila linalotuka, min-ghair ya kutangulizwa jina la Mnyezi Mungu, jambo hilo ni lenye kukatika, au kuwa na barka chache".

Imaan zaidi kuliko kuamini Mnyezi Mungu, na Malaika wake na vitabu vyake, na Mitume yake na kuamini siku ya mwisho na kudra (kheri na shari) zote zikiwa zinatokana na Mnyezi Mungu aliyetukuka.

Na nimekiita: **Maana halisi ya Imaan** nikiamini ya kwamba mara baada ya mtu kukisoma hatakosa kujiona ana lile jicho la tatu ambalo kwa wengi huwa haliwadhihirikii mapema katika uhai, khasa khasa ukizingatia maanani asri hii yetu ya Ishirini ambapo Dini inachukuliwa kama kitu cha kudharauliwa na kisichokuwa na maana
yoyote wala maendeleo kwa ujumla. Na badala yake ikiwa nyimbo za souls, Bolingo na mipira, ambavyo ni vitu vya upuuzi mtupu ndiyo vyaoneka muhimu mno.

Namtakia Rehma na Amani Bwana mbora wa viumbe ambae hana kasoro hata chembe, Bwana Muhammad SAW na Ali zake na Sahaba zake Ajmain, Wal Hamdulillahi Rabbil Alamiin mwanzo na mwisho wake.

Al Faqeer Ahmad Sheikh

بسم الله الرحمن الرحيم

IMAAN

Khatua ya kwanza.

Ukamilifu ni wake yeye Mnyezi Mungu peke yake. Ambaye amejaalia wenye Imaan kamili ndio waliofuzu mafanikio makuu hapa Duniani na kesho akhera. Na Rehma ni juu ya Mtume Muhammad SAW. Mara fikra zetu tuonapo neno **Imaan** hupaza katika nguzo sita kama zilivyo maarufu mwenye vitabu vingi sana kuwa ni :-

a) kuamini Mnyezi Mungu
b) kuamini Malaika wake.
c) Kuamini Vitabu vyake
d) Kuamini Mitume wake
e) Kuamini Siku ya mwisho
f) Kuamini Kudra (Kheri na Shari) yake zinatokana nae Mnyezi Mungu. Na ambaye anaamini hayo kwa jumla huwa tayari anayo **Imaan**.

Na pia anaeamini hivyo huwa ndio **Muumin**. Jee ikiwa jumla ya mambo sita hayo ndio nguzo za Imaan sasa nini na ni kitu gani basi hiyo **Imaan?**

Hili ni suali muhimu mno kwa kila mmoja, kwani hebu na tuchukue mfano wa aya hii tuone nini hukumu yake ili upate kujisahihisha**. Qur an Anfaal 8 : 2.**

إِنَّمَا ٱلْمُؤْمِنُونَ ٱلَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ ٱللَّهُ وَجِلَتْ قُلُوبُهُمْ وَإِذَا تُلِيَتْ
عَلَيْهِمْ ءَايَٰتُهُۥ زَادَتْهُمْ إِيمَٰنًا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٢﴾

"Hakika wanaoamini kweli ni wale ambao anapotajwa Mwenyezi Mungu nyoyo zao hujaa khofu; na wanaposomewa Aya zake huwazidishia Imaan na wakamtegemea Mola wao tu basi"

Katika Aya hii tumesifiwa vya kutosha juu ya Muumuni na tumeona ya kwamba inahitaji mtu huyo kua na :-

i) **Woga wa Mola wake**: kiasi ambacho, hata anapotajwa tu, huwa yeye moyo wake unashituka kwa khushui na kumzidi Imaan yake

ii) **Tawakkul:** ambayo inaonyesha wazi wazi kua mtu huyo (Muumini) daima lazima ayatupe mambo yake yote kwa Mnyezi Mungu.

Na tujiulize ni mara ngapi anapotajwa Mnyezi Mungu Imma ndani ya Redio, ukasikia mtu (hali ni Mwislam) anasema: "Ondosha bwana, sisi hatuko Msikitini hapa, weka taarifa ya habari au fungua mpira au kongo". Jee katika hukumu hii tujiweke katika fungu gani la **Imaan?**

Tukizidi upekuzi hebu tuangalie kuna nini ndani ya Aya hii aelezeayo Mnyezi Mungu? **Qur an Hujurat 49:14-15.**

۞ قَالَتِ ٱلۡأَعۡرَابُ ءَامَنَّاۖ قُل لَّمۡ تُؤۡمِنُواْ وَلَٰكِن قُولُوٓاْ
أَسۡلَمۡنَا وَلَمَّا يَدۡخُلِ ٱلۡإِيمَٰنُ فِي قُلُوبِكُمۡۖ وَإِن تُطِيعُواْ ٱللَّهَ
وَرَسُولَهُۥ لَا يَلِتۡكُم مِّنۡ أَعۡمَٰلِكُمۡ شَيۡـًٔاۚ إِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٞ رَّحِيمٌ ١٤
إِنَّمَا ٱلۡمُؤۡمِنُونَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ بِٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦ ثُمَّ لَمۡ يَرۡتَابُواْ وَ
جَٰهَدُواْ بِأَمۡوَٰلِهِمۡ وَأَنفُسِهِمۡ فِي سَبِيلِ ٱللَّهِۚ أُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلصَّٰدِقُونَ ١٥

"Walisema watu wa majangwani (kumwambia Bwana Mtume Muhammad S.A.W) Tumeamini" (sema uwaambie) "Hamjaamini kweli kweli bado, lakini semeni "Tumesilimu"(Yaani Tumenyenyekea na kufuata aliyokuja nayo Bwana Mtume Muhammad S.A.W)" maana Imaan haijaingia vyema nyoyoni mwenu bado. Na mkimtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hatakupunguzieni chochote katika (thawabu za) vitendo vyenu kwa yakini Mwenyezi Mungu ni msamehevu (na) Mrehemevu."

Wenye kuamini kikweli kweli ni wale waliomuamini Mnyezi Mungu na Mtume wake, kisha wakawa si wenye shaka, na wakapigania Dini ya Mnyezi Mungu kwa mali zao na nafsi zao. Hao ndio wenye kuamini kweli kweli.

Allahu Akbar, hebu tutizame mfano uliopigwa hapo, juu ya sifa ya Muumini ni vipi hukumu yake. Katika Aya hii zaidi ya kuambiwa hao watu wa majangwani kuwa bado hawajaamini ila wamefikia khatuwa ya kuwa Waislam tu, tutaona yapo mambo haya yafuatayo hapa chini:-

1. **Kua Mwislam kwanza:** Ndio kusema hawezi kupata Imaan mtu sharti awe Mwislamu, hii inawafik sana kauli zao Wanazuoni walochunguza Qur an barab-bar na kuona ya kua Imaan na Uislamu ni kama **kifua** na **mgongo** hawezi kua mtu na Imaan bila kua ni Mwislam, kama isivyowezekana kua mtu Mwislam bila kuwa na Imaan.
2. **Twaa ya Mnyezi Mungu na Mtume wake:** Yaani katika kumtii Mnyezi Mungu juu ya kutekeleza kila ambalo ameliamrisha na kuacha kila ambalo amelikataza na pia vivyo hivyo kwa sunna za Bwana mtume SAW kwani bil kul sio kwamba kazibuni yeye, bali ukizitafiti sana utakuta ni amri ya Mnyezi mungu, kwa ushahidi wa wahyi uliofunuliwa (kwake). **Qur an Nnisaa 4 : 80.**

مَّن يُطِعِ ٱلرَّسُولَ فَقَدۡ أَطَاعَ ٱللَّهَۖ وَمَن تَوَلَّىٰ فَمَآ أَرۡسَلۡنَٰكَ عَلَيۡهِمۡ حَفِيظٗا ٨٠

"Mwenye kumtii Mtume amemtii Mwenyezi Mungu (kwani anayoyaamrisha Mtume yametoka Kwa Mungu). Na anayekengeuka (anajidhuru Mwenyewe). Hatukukupeleka wewe kuwa mlinzi juu yao; (wakipotea ulaumiwe wewe .La. Hatuku fanya hivyo)".

Na vile vile katika: **Qur an Suratil Najim 27:4.**

إِنَّ ٱلَّذِينَ لَا يُؤۡمِنُونَ بِٱلۡأٓخِرَةِ لَيُسَمُّونَ ٱلۡمَلَٰٓئِكَةَ تَسۡمِيَةَ ٱلۡأُنثَىٰ ٢٧

"Kwa hakika wale wasioamini AkherTumewapambia vitendo vyao (vibaya, wakaviona vizuri), basi kwa hivyo wanaduaa tu (katika hayo mabaya yao)"

1. **Yaqin:**Yaani hatokuwa mtu na sha a yeyote juu ya Imaan yake kua ni kweli au uwongo.

Jee wangapi leo hufikwa na majanga wakavunjika moyo kiyasi cha kusema Mnyezi Mungu hayuko kabisa? (Fal-Iyadh Billah)

.

2. **Jihadi ya mali na nafsi**: Yaani kua na Imaan utaona ya kua inahitaji sana kwa mtu kupigania Dini ya Mnyezi Mungu kwa mali na nafsi yake mtu.

Jee, ambao wana mafedha kem kem wameyarundika tu, ni nini hukumu zao?. Katika kuzidi kuchekecha hebu na tutizame zaidi ndani ya

Aya hii iliopo kwenye juzuu ya 18: **Qur an Mu'minun 23:1-6**

قَدْ أَفْلَحَ ٱلْمُؤْمِنُونَ ﴿١﴾ ٱلَّذِينَ هُمْ فِى صَلَاتِهِمْ خَٰشِعُونَ ﴿٢﴾
وَٱلَّذِينَ هُمْ عَنِ ٱللَّغْوِ مُعْرِضُونَ ﴿٣﴾ وَٱلَّذِينَ هُمْ لِلزَّكَوٰةِ فَٰعِلُونَ ﴿٤﴾
وَٱلَّذِينَ هُمْ لِفُرُوجِهِمْ حَٰفِظُونَ ﴿٥﴾ إِلَّا عَلَىٰٓ أَزْوَٰجِهِمْ أَوْ مَا مَلَكَتْ
أَيْمَٰنُهُمْ فَإِنَّهُمْ غَيْرُ مَلُومِينَ ﴿٦﴾

"Hakika wamefuzu walioamini (waislamu) ambao katika sala zao hua wanyenyekevu, na ambao hujiepusha na mambo ya kipuzi. Na ambao nguzo za zaka wanazitekeleza na ambao tupu zao wanazilinda isipokuwa kwa wake zao au kwa (wanawake) wale iliyowamiliki mikono yao ya kuume (kulia) basi hao ndio wasiolaumiwa".

Aya hizi zimezidi kutusogeza mbali sana katika taabiri ya Imaan, na kutuonyesha wazi wazi kua, zaidi ya kuamini Mnyezi Mungu, malaika, vitabu na mitume yake, na kuamini siku ya mwisho na qudra, ili kuikamilisha Imaan ni lazima kuwepo mambo mengi yaliyo muhimu sana sana kila moja kwa upande wake na sifa zake. Ndani ya Aya hizo tunapata mambo makubwa yafuatayo:- Unyenyekevu ndani ya sala: Hii ni kwa sababu asiyekua na huo unyenyekevu basi wazi wazi huyo si muumin bali ni mnafiki.na khasa kwa mazingatio ya Aya ya **Qur an Suratil Tawba 9:54.**

وَلَا يَأْتُونَ ٱلصَّلَوٰةَ إِلَّا وَهُمْ كُسَالَىٰ ...

"…..Na wala hawafiki mahala pa kusalia ila katika hali ya uvivu…"

Vile vile Aya hii:- **Suratul Maidah 5:58.**

وَإِذَا نَادَيْتُمْ إِلَى ٱلصَّلَوٰةِ ٱتَّخَذُوهَا هُزُوًا وَلَعِبًا ۚ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَّا يَعْقِلُونَ ﴿٥٨﴾

"Na mnapoita kwendea (mnapoadhini) wanaifanyia mzaha na mchezo hayo ni kwa sababu wao ni watu wasio na akili."

5. **kujiepusha na Upuuzi.**
6. **Ulinzi wa tupu:** Ndio kusema wazi kabisa ya kuwa muumin hutamkuta akizini au akilawiti au kulawitiana.

Hadithi ya bwana mtume S.A.W inafahamisha ya kua hana Imaan ambae anazini

مامن مومن يزني و هو مؤمن

"Hawi Muumin anazini, zama zile akizini, na hali ya kua Muumin."

Hii inaonyesha ya kua Imaan humtoka kabisa na ikiwa ni hivyo, basi ni sahihi hadithi yake nyingine kua Imaan imeletwa ikiwa ni uchi. Au Pia katika hukumu ya tupu amesema Bwana Mtume S.A.W.

ملعون من عمل عملا قوم لوط

"Amelaaniwa afanzae amali ya Qawmu-Luut"

Amma kivyote vyote afanzae na afanzwae. Jee hatuelewi ni nini walifanzwa hao watu wa Sayyidna Luut waliokuemo katika mji wa Sodom na Gomora, na leo ni wangapi wanaotimiza Liwa-t hata kwa wake zao licha waume peke yao?

7. **Kutekeleza Amana na Ahadi:** Hapa tunaona ya kua ili ipatikane Imaan ni lazima Muumin awe mtekelezaji Amana Kama alivyo lihozi jina hili Bwana mtume S.A.W tangu akiwa mdogo- "Muhammad El-Amiyn."

Leo na tujiulize ni mara ngapi tunakhini Amana za watu jee si wanafiki wafanzao hivyo, kwa hadithi ya Bwana Mtume S A W? Alama za mnafiki ni tatu:-

a) Anapozungumza husema uongo.

b) Anapoahidi hukhalifu na

c) Anapoaminiwa ukhini.

Jee, ikiwa hadithi hii haitupambi (na haiwezekani kabisa isitupambe). Jee hata Aya ya Mnyezi Mungu. **Qur an Nisaa 4:145.**

إِنَّ ٱلْمُنَٰفِقِينَ فِى ٱلدَّرْكِ ٱلْأَسْفَلِ مِنَ ٱلنَّارِ وَلَن تَجِدَ لَهُمْ نَصِيرًا ﴿١٤٥﴾

"Bila shaka wanafiki watakuwa katika tabaka ya chini kabisa katika moto. Hutamkuta kwa ajili yao msaidizi (yeyote)."

Na eti badala ya Muumin tunawasifu wasiokua muumin kua ndio watekelezaji wa Amana na Ahadi. Tuikumbuke hadithi ya Bwana Mtume S.A.W:

"Hana Imaan asiekua na Uaminifu na hana Dini asiekua na Ahadi."

8.**Kuhifadhi**

sala: ⓪⓪ ⑤⓪ ❸☙❻⓪ ②❶☙ ❶❶④⓪⑤ ☙❶⓪⑦❶❶❻☙ ⑩☙③☙ ☙❶⓪☙ ⑩⓪②❶ ④⑥①☙ ❻☙⓪☙⓪ ❺☙ ②❶☙

ni lazima kwake kwa ushahidi wa **Qur an Nnisaa 4 :103.**

إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ كَانَتْ عَلَى ٱلْمُؤْمِنِينَ كِتَٰبًا مَّوْقُوتًا ﴿١٠٣﴾

"… Kwa hakika sala kwa waislam ni faradhi iliyowekewa wakati makhsusi……"

Pia katika **Qur an 107: 4 -5.**

فَوَيْلٌ لِّلْمُصَلِّينَ ﴿٤﴾ ٱلَّذِينَ هُمْ عَن صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ ﴿٥﴾

"Basi adhabu itawathubutikia wanao sali ambao Wanapuuza (maamrisho ya) sala zao (kama Kuwafanyia wema viumbe wenzao)."

Na huo moto (Wa-Waylu) ni sehemu tu ambayo ipo Jahannam lau linaekwa karibu yake jabali la Duniya litayayuka kwa uharara wake tu, si kwa moto wenyewe. Ama kwa kauli ya Bwana Mtume S.A.W kua

"Sala ni (Nuru) Mwangaza wa Imaan"

Tabaan, mtu Muumini daima itakua ni taabu juu yake kuiacha.

Miongoni wa amali alizozifanya sana Bwana Mtume S.A.W ni kusali. Mpaka kufikia hapa tumeshaona ya kwamba tunazidi kuwa mbali zaidi na jinsi vile tunavyoijua Imaan, na hakika si vingine kila tunavyofunua Msahafu wa Mnyezi Mungu kupekua Aya ambayo imetaja kitu kidogo juu ya Imaan tunaona utajo wake huo unakua tofauti na ulokwisha pita, na isitoshe unatueleza kitu kingine kabisa na kigeni juu ya Imaan na sifa za Muumini, pia mpaka hapa hatujafikia Aya ambayo imeelezea juu ya nguzo sita za Imaan tunayoijua sana tangu utotoni mwetu. Ni zaidi kuliko vile tunavyoielewa?. Lazima ni zaidi.

Mwenye kutafuta hua hajui kuchoka, ama sivyo huwa si mtafutaji kweli. Hapa tuna dalili nyingine Inayotufahamisha machache zaidi ambayo mmeshapata kuhusu Muumini:- **Qur an 2:1-5**

الٓمٓ ﴿١﴾ ذَٰلِكَ ٱلۡكِتَٰبُ لَا رَيۡبَۛ فِيهِۛ هُدٗى لِّلۡمُتَّقِينَ ﴿٢﴾ ٱلَّذِينَ يُؤۡمِنُونَ
بِٱلۡغَيۡبِ وَيُقِيمُونَ ٱلصَّلَوٰةَ وَمِمَّا رَزَقۡنَٰهُمۡ يُنفِقُونَ ﴿٣﴾ وَٱلَّذِينَ
يُؤۡمِنُونَ بِمَآ أُنزِلَ إِلَيۡكَ وَمَآ أُنزِلَ مِن قَبۡلِكَ وَبِٱلۡأٓخِرَةِ هُمۡ يُوقِنُونَ
﴿٤﴾ أُوْلَٰٓئِكَ عَلَىٰ هُدٗى مِّن رَّبِّهِمۡۖ وَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡمُفۡلِحُونَ ﴿٥﴾

"Alif Lam Mym. Hiki ni kitabu kisichokua na shaka ndani yake ni uwongozi kwa wamchao Mwenyezi Mungu. Ambao huyaamini yasionekana (madam yamesemwa na Mwenyezi Mungu na Mtume wake) na husimamisha sala na hutoa katika yale tuliyowapa. Na ambao wanaamini yaliyoteremshwa kwako na yaliyoteremshwa kabla yako na wanaamini (kuweko) akhera. Hao wako juu ya uwongozi utokao kwa Molo wao, na hao ndio wenye kuongoka."

Tukichambua Aya hii tunapata mambo muhimu kuhusu Imaan kama ifuatavyo:-

a) Wenye kumcha Mnyezi Mungu: Hii inaonyesha wazi kua yeyote anaemcha Mnyezi Mungu kua Muttaqi yaani mwenye kumcha Mnyezi Mungu kikweli. Na huko kumcha kwenyewe ni kumuogopa Mnyezi Mungu kikweli, na lau kumuogopa huko sio kama tunavyoogopana baadhi yetu kwa baadhi labda kwa sababu fulani Fulani ambazo ni tofauti kabisa.

Mathalan sisi tunatokea kuogopana kwa sababu mmoja ana silaha za kutisha, au cheo au kifua kipana; laa woga wa Mnyezi Mungu umo ndani ya mja kutekeleza yale ambayo Mola amemwamrisha nayo, na kuacha yale ambayo amemkataza nayo.

b) Na hakika si vingine nyoyo ambazo ziko mbali na rehma ya Mnyezi Mungu hakuna kuliko nyoyo (mioyo) migumu. Mnyezi Mungu ametuambia: **Qur an Baqarah 2:7.**

خَتَمَ ٱللَّهُ عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ وَعَلَىٰ سَمْعِهِمْ ۖ وَعَلَىٰٓ
أَبْصَٰرِهِمْ غِشَٰوَةٌ ۖ وَلَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٧﴾

"(Kama kwamba)Mwenyezi Mungu amepiga muhuri juu ya nyoyo zao na juu ya masikio yao; na juu ya macho pana kifuniko; basi watakua na adhabu kubwa."

Vile vile katika: **Qur an Al Mutaffifyn. 14.**

كَلَّا ۖ بَلْ ۜ رَانَ عَلَىٰ قُلُوبِهِم مَّا كَانُوا۟ يَكْسِبُونَ ﴿١٤﴾

"Sivyo hivyo bali yametia kutu juu ya nyoyo zao (maovu) waliyokua wakiyachuma".

.

Amesema Bwana Tirmiydh RA, mmoja katika wanavyuoni wakubwa ambaye amesimulia hadithi nyingi sana za Bwana Mtume S.A.W:

"Uhai wa Moyo ni Imaan, na Mauti ya Moyoni kufru, na sihha yake ni Twa-a, na maradhi yake kuyaandama maasi, kuamka kwake ni dhikri na kulala kwake ni Ghafla."

Kwa hadithi hii ambayo inayo mengi yaliyogusiya yale ambayo sasa hivi tumeyataja hapo juu inaonyesha wazi kua (ili kujiandaa) Imaan ni mkusanyiko wa mambo mingi. Yaani Mnyezi Mungu si wa kuonekana kwa macho kwa sababu lau tungemuona tusinge kuwa hai sote.

Yeye amejielezea tu juu ya sifa zake, jinsi vile alivyo, na jinsi sifa zake zilivyo, basi mtu ikawa anaamini otomatiki bila ya kutaka jambo lolote la kuthibitisha au kupima.

Kuamini kwa ghaib huko (ni mfano ule wa existing fact) unaamini kuwepo kwa moto, ajali ya gari, mnyama mbaya mara baada kupewa habari hiyo na ambaye umekutana nae akitokea uwendako. Ukweli unabaki nawe kila hatua yako kuelekea penye tukio mpaka kulifikia, ambako unathibitisha kwa macho jambo lile ulilopewa habari yake hapo nyuma, kuanzia ulipopewa habari ya moto na bila ya kuona hata ule moshi, ajali ya gari na bila kuona gari yenyewe au wahusika wake, mnyama na bila ya kumsikia wala kumuona, kipande chote hicho ikiwa Imaan ndani mwako na mategemeo ya dhati kua tukio lile lipo tu.

Hali kadhalika kuyaamini ambayo yamefichika miongoni mwa vitu kama pepo, moto, sirat, mizani, kiyama, kufufuliwa na kama hivyo ni mambo hakika yake inatangulia kuwepo moyoni na mwenye itikadi (**Existing fact)** kabla.

Ama kiakili tu kule kuamini Mnyezi Mungu kwa ghayb bila ya kuhitaji kumuona kwa macho kunatosha, kwani baada ya kujisifu kwake kua hafanani na kitu chochote isingeleta maana yeyote maalumu na mtu hangewaza kuifahamisha kwa mwingine. Bin Adam angezingatia suala la 'JUA' tu. Ingetosha kujiamuli mwenyewe kuwa ni upumbavu kudai kumuona Mnyezi Mungu ili kufidia hoja kamili ya kuamini. Kwani ni Dhahiri kuwa aliyemudu kuliumba bila kudhurika. na lile joto lake (11,000,000 degree, wanavyodai wanasayansi) Ingehitaji zaidi ya mwenda wazimu kutamani kumuona kwa macho Matupu (Naked eye's or by other reliable source) au kwa msaada wa chombo chochote kingine madhubuti.

b) Kusimamisha sala: Mara nyingi sala imekokotezwa sana na Kwa kweli baada ya shahada katika Uislam hakuna amali ya pili iliyo kubwa mno kuizidi. Umuhimu wake unatudhihirikia wazi kutokana na hadithi na sifa nyingi juu ya Bwana Mtume S.A.W kama kule kuvimbwa na miguu kwa ajili ya kusimama usiku kusali. Au vile Mnyezi Mungu Sub-hana wa Taala alivyomnadia. **Qur an Muzzammil 73:1-4.**

c)

يَٰٓأَيُّهَا ٱلْمُزَّمِّلُ ﴿١﴾ قُمِ ٱلَّيْلَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٢﴾ نِّصْفَهُۥٓ أَوِ ٱنقُصْ مِنْهُ قَلِيلًا
﴿٣﴾ أَوْ زِدْ عَلَيْهِ وَرَتِّلِ ٱلْقُرْءَانَ تَرْتِيلًا ﴿٤﴾

"Ewe Mwenye kujigubika Maguo simama kwa Ibada zako za usiku ila muda mchache tu nusu yake, au punguza kidogo au izidishe, na usome Qur-an vilivyo"

Huu ni uthibitisho tosha kabisa juu ya Bwana Mtume SAW kupendelea kusali. Isitoshe sala hiyo, ni mkusanyiko wa Ibada za Malaika wote kwa jumla na ilifaridhiwa siku ile aliporudi miraji baada ya kwisha waona hao Malaika wakisali, Mnasab na muwafak 27 Rajab, mwaka wa kumi tangu kubaithiwa, na wala haikusaliwa asubuhi siku ile. (Aliporudi toka miraji).

Utowaji – Muumini kama ilivyo hadithi ya Bwana Mtume S.A.W. kuwa **"Bakhili ni Adui wa Mnyezi Mungu"** Yeye hutoa kile ambacho ameneemeshwa na Mola wake, haweki kitu, au kuwa na sifa ya kiunyimi. Bwana Mtume S.A.W ametuambia pia: –

"Muumini ni yule ambae hutoa sadaka kile anachokipenda nafsi yake"

Hii ni kutokana na kauli ya Mola aliposema: **Qur an Al Imraan. 3:92.**

لَن تَنَالُواْ ٱلْبِرَّ حَتَّىٰ تُنفِقُواْ مِمَّا تُحِبُّونَ

"Hamtoweza kufikia wema mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda".

e). (Kuamini) Imaan juu ya yale ambayo yameshushwa kwa walio kabla ya Bwana Mtume S.A.W.

f). Yaqin kuwepo kwa siku ya mwisho. Hii imegusia vile ilivyotajwa mwenye nguzo za Imaan nguzo yake ya tano. Tangu tuanze kuelezea hadi fika yetu hapa ni sehemu hii tu ambayo imeelezea jambo moja la kulingana na yale yalitajwa juu ya nguzo ya Imaan.

Ni juu yetu kujiuliza ikiwa mpaka sasa tumepata sifa Kemkem kama zilivyo chini hapa kwa ujumla wake juu ya Imaan ni nini Khasa maana yake khalisi.

Sifa za muumin kwa kadri ya ubainifu tuliopata mwenye baadhi ya Aya chache tu hizi na falau ziko nyingi mno ndani ya Qur an ni kama hizi:

1. **Taqwa**
2. **Tawaqul**
3. **Uislam**
4. **Twaa**
5. **Yaqin**
6. **Jihadi ya Mali na Nafsi**
7. **Unyenyekevu mwenye sala**
8. **Hifadhi ya tupu**
9. **Kutekeleza Amana na Ahadi**
10. **Kuhifadhi sala**
11. **Utowaji**
12. **Kuyakubali ambayo yaliteremshwa kwa waliomtangulia Bwana Mtume Muhammad Sallal Lahu Alyh Wasalam.**

Amma yale ambayo tumeyafahamu toka kwenye suratil Hujurat Aya ya kumi na nne na tano, inatudhihirikia wazi ya kua Imaan huwemo ndani ya Moyo wa mtu Muumin. Na ni Mnyezi Mungu ambaye huiweka lakini huwa ni kwa sharti ya mtu kumtii Mnyezi Mungu na Mtume wake. Na madhali imeswiri kuwemo ndani ya moyo inakuwa ni kitu cha mwanzo kupatwa na Ghafla. Basi Ghafla hiyo isipoamshwa huwa ni jambo la kupita, la fikra toka hapo isiporudiwa na Mnyezi Mungu pamoja na kuanza kutumika au kusarifika kama ada yake, basi huwa ni lazima kuingia kwenye jambo la azma tu, ambayo khatua hii hapa isipokingwa barabara, ni lazima ituke kwenye maasi tu, na toka hapo moyo usipopata njia ya toba sawa sawa lazima utakua moyo sugu na mgumu kama jiwe, na toka hatua hii, usipopata maonyo huswiri kuwa na tabia ya kupigwa muhuri. Katika hatua mbili hizi za mwisho kuna msemo juu yake. Mtungaji kitabu maarufu cha

"Zubad" amesema:-

> **"Hakika ya matamanio ya moyo pamoja na kutenda dhambi huwa ni sababu mbili za lazima kuufanya moyo kuwa mgumu".**

IMAAN

Katika kuifunua Imaan vile inavyostahiqi kujulikana kwake hasa, tumegusia kimukhutasari tu juu ya maelezo yaliyopita katika khatua ya kwanza (Hii siyo khatua ya sheria ya Mnyezi Mungu laa, bali ni kule kupendelea kuyagawanya maelezo yake vifungu vifungu tu). Katika hii khatua ya pili tumependelea zaidi tutizame vile tunavyoijua kidogo Imaan kinjia ambayo kwa hakika ni nguzo zake hiyo Imaan kama tulivyofunzwa mwenye mafunzo ya Fiqhi. Takriban mwenye vitabu vidogo dogo kama vile Risala, Arshadul Muslim, Safina na mfano wa hivyo ambavyo si muhimu kuvitaja vyote, vimeelezea kama hivi:- Nguzo za Imaan ni sita, ya kwanza ni:

kumuamini Mnyezi Mungu
Kuamini Malaika wake.
Kuamini Vitabu vyake.
Kuamini Mitume yake.
Kuamini siku ya mwisho.
Kuamini Kudra – kheri yake na Shari yake zote zinatokana na Mnyezi Mungu.

Amesema Bwana Mtume S.A.W (katika hadithi ambayo ameipokea na ilisemewa na Seyyidna Omar Radhi za Mnyezi Mungu juu zake): “Siku moja tulipokuwa tumekaa na Bwana Mtume S.A.W alituchomozea mtu mgeni aliyevaa nguo nyeupe sana, alikua na nywele nyeusi mno, hakuna kati yetu aliyemjua wala aliyemuona na athari yoyote kama ni msafari. Alikuja moja kwa moja mpaka pale alipokua amekaa Bwana Mtume S.A.W akakaa mkabbala nae hali ya kuambatanisha karibu maundi yake na ya Bwana Mtume S.A.W kisha akaweka viganja vyake juu ya mapaja ya Bwana Mtume S.A.W na kumuuliza “Ya Rasulal Llah. (Ewe mjumbe wa Mnyezi Mungu) nini Uislam? (Yaani nipe habari juu ya Uislam).” Bwana Mtume S.A.W akamjibu. “Ni kukiri kwa moyo na kubaini kwa ulimi ya kuwa hapana apasae kuabudiwa kwa kweli illa Mnyezi Mungu na mimi ni mtumwa wake na mjumbe wake, Kusali sala tano kila moja kwa wakati wake makhsusi, kutoa Zaka kwa mwenye mali, kufunga mwezi wa Ramadhani, kuhiji Makka (Au kukusudia nyumba tukufu ya Mnyezi Mungu kwa ibada) kwa mwenye uwezo wa kwenda falau mara moja katika umri”.

Yule mgeni akasema “Sadakta”, yaani umesema kweli, tukastaajabu kuona anauliza yeye na kusadikisha yeye, kisha akaulizi tena : “Nini Imaan?”. Bwana Mtume S.A.W. akamjibu ni kuamini Mnyezi Mungu na Malaika wake, na Vitabu vyake na Mitume yake, na kuanimi Siku ya mwisho, na Qudra, yaani kheri yake na shari yake zote zinatoka kwake yeye Mnyezi Mungu Azza wa Jalallu.

Alipomaliza masuali yake (ambayo yalijumuisha pia suali la **Ihsan),** yaani kule kumuabudu Mnyezi Mungu kama ambae unamuona, na ikiwa humuoni basi yeye anakuona, na pia suali la Kiyama, na dalili zake kama zilivyo mashuhuri kama vile kupitana katika majenzi marefu marefu mfano labda Sky Scrapers ambazo hazikuwepo zama zile za Bwana Mtume S.A.W. watu kwenda uchi, (yaani kwa mwanamke asiyekuwa mfanyakazi basi kiwiliwili chake chote kwa wafaao kumuona na kasoro ya uso wake na vitanga vya mikono zama za kusali). Mjakazi sawa na mume baina ya kitovu na magoti na nyingi ya dalili za kiyama aloelezea Bwana Mtume S.A.W. nyingi zikiwa zimeshuhudiwa moja baada ya nyingine hadi hii karne ya ishirini.Yule mgeni Aliondoka na hakuna alojua ameenda wapi. Bwana Mtume S.A.W. aliwauliza masahaba “Mnamjua aliekua akiuliza, wakamjibu “Allahu wa Rasuluhu Aalam” akawaambia ni (Seyyidna) Jibril (Malaika muhusika na Wahyi) ambaye aliwajia ili kuwafunza Dini yao (Islam).

Katika hadithi hii tunaona ya kua Seyyidna Jibril Aleyhi Salam, hakuuliza masuali zaidi kuliko haya ya Uislam Imaan na Ihsan, (ambalo lilikuwa kati yake, ila tumefupiza tu) kwa hiyo ni wazi ya kuwa ni muhimu sana, ni wapi tungepata vizuri maelezo ya Imaan kama ilivyo hapa au kama si pale Mnyezi Mungu aliposema:

Baqarah Qur an 2 : 285.

ءَامَنَ ٱلرَّسُولُ بِمَآ أُنزِلَ إِلَيۡهِ مِن رَّبِّهِۦ وَٱلۡمُؤۡمِنُونَۚ كُلٌّ ءَامَنَ بِٱللَّهِ
وَمَلَٰٓئِكَتِهِۦ وَكُتُبِهِۦ وَرُسُلِهِۦ لَا نُفَرِّقُ بَيۡنَ أَحَدٖ مِّن رُّسُلِهِۦۚ وَقَالُواْ سَمِعۡنَا
وَأَطَعۡنَاۖ غُفۡرَانَكَ رَبَّنَا وَإِلَيۡكَ ٱلۡمَصِيرُ ٢٨٥

"Mtume ameamini yaliyoteteremshwa kwake toka kwa Mola wake, na Waislam (waameamini hayo pia) wote wamemuamini Mwenyezi Mungu na Malaika wake, na Vitabu vyake, na Mitume yake, (Nao husema) hatutofautishi baina yoyote katika Mitume yake na husema "Tumesikia na Tumetii" (Tunakuomba) Msamaha wako Mola wetu na marudio ni kwako."

Katika Aya hii takriban imekusanya maelezo mazuri Kuhusu Imaan, kwa mnasaba wa sehemu yetu ya pili tulioiita **Khatua ya pili**, lakini tutaona pia haijatupa wazi wazi kabisa maana ya Imaan, na hivyo ndivyo ulivyo mtindo wa Qur an, ili kusudi tu mtu uwe kila mara unayo hamu ya kutafuta zaidi. Na laiti Mnyezi Mungu jinsi anavyomuelewa Bin Adam, angemuekea kila kitu hapo hapo, ni wazi kabisa kungekosekana haja ya kujishughulisha ambapo ndio haja kubwa kabisa ya kuumbwa mtu.

IMAAN

Khatua ya tatu.

Nini maana yake:

Tumefikia khatua muhimu na iliyo na maana kabisa katika kijitabu chetu hiki. Na lau tangu mwanzo, ulikuwa na fikra ambazo kwa kweli ni lazima tuziite, nyepesi mno katika kuijua na kuitambua Imaan nini maana yake fikra zako hizo nasaha juu yako na iwe zimefika mwisho wa kutoshekwa kwake huko, na iwe ndio mwanzo wa kupandwa na ham, mapenzi na ashqi yenye nguvu kutaka kuipapia ilmu ya Imaan tangu leo.

Lau kuna waliowahi kumwendea Bwana Mtume S.A.W. na kumuuliza mara nyingi: "Ya Rasulal Lahi nifanye nini zaidi ili niwe katika wachaji wa Mnyezi Mungu?" Na aliwajibu: "Muamini Mnyezi Mungu na utosheke na kufanya kwako mambo mema". Lakini utaona huko huko kuamua kumwamini Mnyezi Mungu sio rahisi kama yalivyo maneno yake hayo mawili mataatu tu ".. Kumu-amini…".

Nimejaribu kadri nilivyoweza kulieleza neno Imaan kwa wajihi mbili tatu mbali mbali ili itufahamikie kwa jumla ya neno moja.

WAJIHI WA KWANZA:

Katika moja ya hadithi nyingi alizosimulia Bwana **Baihaqiyu R.A** ni ile isemayo kwamba aliulizwa Bwana Mtume S.A.W. Nini Imaan? Akasema: "Imaan ni Ikhlaas" (Yaani kule kumtakasa Mnyezi Mungu bila kumshirikisha na kumfananisha na kitu chochote kile. Ndio kusema Mnyezi Mungu mmoja tu. Mnyezi Mungu tu ndiye anayestahiki kukusudiwa na viumbe vyake vyote. (Kwa kumuabudu kumuomba kila kitu na kumtegemea kwa kila kitu), kwani si vingine ila ni kuwa mwanadamu hana hila yoyote ya kutumia, ili afanye (Twaa) wala nguvu ya kufanya maasi ila kwa kutaka Mnyezi Mungu. Hakuzaa, wala hakuzaliwa wala hafanani na hata mmoja). Na pia akaulizwa: "Nini maana ya Kukiri?".

Bwana Mtume S.A.W. akasema "Ni kukubali, na kuamini kweli kweli." Kama tulivyokwisha ona katika Aya ile ya Suratil Hujurat, hao ndio wanaoamini kweli kweli. Tukiendelea zaidi katika Wajihi wa pili tutaona ya kuwa huko kuamini kweli kweli kulikodhamiriwa kuwa ndio Imaan kwa maana yake yenye kuambatana na huu wajihi wa kwanza katika dhati ya maana ya Imaan,

(tutaona ni) kuwa na Itiqadi kwa mkato, juu ya kupatikana Mnyezi Mungu muumba wa kila kitu, na kutomuogopa asiyekuwa **Yeye** Jalla jalalu na pamoja na kufanza amali zote kwa njia ya Lillahi, na njia iliyo njema toka Moyoni mwake mtu.

WAJIHI WA PILI.

Seyyidna Omari Radhi za Mnyezi Mungu juu yake khalifa wa pili wa Waislam baada ya kutawafu Bwana Mtume S.A.W. na ambae anakutana na Bwana Mtume S.A.W. kwa babu yao Ibni Adiyyi Ibni Kaab kama alivyoonyesha wazi Al Marhum Sheikh Abdallah swaleh El-Farsy kwenye kitabu chake "Maisha ya Nabii Muhammad-S.A.W."

Imepokewa hadithi toka kwa Bwana Mtume S.A.W. kuwa amesema mjumbe wa Mnyezi Mungu S.A.W:

> **"Haikubaliwi Imaan bila ya Amal, na kama hivi haikubaliwi Amal bila Imaan".**

Hadithi hii ni yenye kukubaliana kabisa na Aya ile inayo wakhusu watu wa majangwani. Na mtapomtii Mnyezi Mungu na Mjumbe wake hatakupunguzieni chochote katika thawabu za vitendo vyenu. Na Mnyezi Mungu ni Msamehevu na Mrehemevu. Na midam hadithi yeyote ifikapo hadi ya kukubaliana kabisa na Aya ya Qur an takatifu, laa shaka hadithi hiyo ni nzuri kwani kabla ya kutawafu Bwana Mtume S.A.W. alishatuambia kuwa ametuachia vizito viwili, **"Qur an" na "Sunna".** Sunna zake zimo mwenye hadithi zake nyingi zisizo idadi kwani huna utapohitaji ukakosa hadithi za Bwana Mtume S.A.W. laa ndani ya Biashara. Zarra-a, Twibba, Walla, Umakanika na kazi nyingine. Imaan pia ni Amal ya moyo. Kwa sababu huo huo moyo ndipo pahala Mnyezi Mungu anapopatizama sana zaidi kuliko popote pa mwanadamu. Mnyezi Mungu kwa hakika, hatazami sura zenu wala hatazami mali zenu. Bali Mnyezi Mungu anatazama mioyo yenu na vitendo vyenu.

Pia Bwana Mtume S.A.W. amesema:

> **"kumjua Mnyezi Mungu kwa moyo pamoja na kukiri kwa ulimi, na kufanza Amal kwa nguzo zake yaani kule kuitekeleza Ibada yako mtu vile ipasavyo".**

Hadithi hii inakubaliana na kuwa kwake **Imaan baatin** (Yaani kitu cha ndani kisichoweza kuonekana na yeyote zaidi ya Mnyezi Mungu), na Uislam kitu cha **dhahir,(** nje wazi ambapo mwingine yeyote anaweza kukiona), ndo kusema –Vitendo vya mtu vikiwa ni vya kiislam hata akiwa si Mwislam atajulikana na kutambulikana kuwa Mwislamu.

Hapa, mualifu wa kitabu **Rawdhatus Salik**, anasema, huko kuamini ni moyoni ama mwenye kukiri kwa Ulimi min-ghairi ya kuamini mbele ya watu tu, lakini mbele ya Mnyezi Mungu ni kafiri. Na kadri wanazuoni walivyochunguza wameona Imaan ni **Martaba nne:-**

i) Imaan ya Alil-Fanaa: Yaani watu ambao wamezama ndani ya kum-pwekesha Mnyezi Mungu, mpaka kufikia kuwa hawaoni chochote mbele yao isipokuwa Mnyezi Mungu tu mmoja. Hao huona kwa jicho la moyo ule Uungu khasa na kutosheka min-ghairi ya kuuliza chochote ili kutaka utulivu wa moyo.

ii) Imaan ya waliokaribishwa: Yaani Muqarabin, watu hawa wanatopewa na kule kuamini Mnyezi Mungu mmoja na kumpwekesha , Tawhidi mpaka imekuwa ni tabiya iliyowavaa ndani kwa ndani na kufikia kuona ambayo jicho la kawaida hata kidogo halioni. Hao hawana la kuogopa isipokuwa Mnyezi Mungu, hawatumai chochote isipokuwa Mnyezi Mungu, wala hawana la kupenda zaidi kuliko Mnyezi Mungu.

iii) Imaan ya kuenea: Hawa ni muumini kwa nyoyo zao na kukiri kwa ndimi zao ila wana kasoro Ihama za wengi wanaosema: "Fuata ninayo kwambia usitizame vitendo vyangu".

Qur an :Baqarah 2:8.

وَمِنَ ٱلنَّاسِ مَن يَقُولُ ءَامَنَّا بِٱللَّهِ وَبِٱلْيَوْمِ ٱلْأَخِرِ وَمَا هُم بِمُؤْمِنِينَ ﴿٨﴾

"Na katika watu wako (wanafiki wasemao)
tumeamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho,
na hali ya kuwa wao si wenye kuamini".

iv) Imaan ya unafiki: Martaba hii ndio wale ambao watu wanawatambua kuwaWaislamu kumbe Mnyezi Mungu anawajua zaidi kwa sababu yeye anaelewa ya ghaib.

Tukiendelea katika Wajihi wa pili tunaona ya kuwa Imaan maana yake ni: "Kukiri kwa ndimi na kuitikadi kwa moyo kule kumpwekesha kwake Mnyezi Mungu, na sifa zake, pamoja na yote yaliyokuja toka kwake, ikiwa ni pamoja na vitabu, Mitume na
Malaika".

WAJIHI WA TATU.

Imaan ni johari ya nafsi ambayo umpatia mtu makamu matukufu na kumwezesha kuona ule uzuri wa Mnyezi Mungu kwa macho yake ya ndani ikawa raha aionayo yeye, mwengine katika watu haioni. Na ni siri toka kwa Mnyezi Mungu juu ya mja wake.

Imaan maana yake **ni ngome saba**, ambazo haziwezi kabisa kabisa kuvunjika kama alivyokwisha kusifia mwenyewe Subhana Wa Taala. **Quran: Hijr. 15:42**

إِنَّ عِبَادِي لَيْسَ لَكَ عَلَيْهِمْ سُلْطَانٌ إِلَّا
مَنِ اتَّبَعَكَ مِنَ الْغَاوِينَ ﴿٤٢﴾

"Hakika watumwa wangu, wewe (Iblisi-lla-in) hutakuwa na mamlaka (nguvu) juu yao, isipokuwa wale wenye kukufwata (kwa khiyari zao) katika hao wapotofu".

NGOME YA KWANZA

Yaqin:

Aliulizwa Bwana Mtume S.A.W. juu ya Yaqin akasema:

"Ni kumwamini Mnyezi Mungu kweli kweli, ikiwa ni pamoja na kuitaqidi kuwa ni mwenye kupatikana na kutomuogopa asiyekuwa yeye."

Amesema mtungaji wa kitabu **"Zubad"** jambo la kwanza lililomlazimu Mwana Adam ni kumjua Mnyezi Mungu kwa **yaqin.** Kisha ni kutamka shahada mbili ili ipate kufaa au iwe sahihi ile Imaan.
Hakika si kingine yaqin ikikaa sawa na kutawala moyo wa mtu, basi vilivyofichika usoni huwa bayana mbele yake.

Yaqin ni Ibara ya nguvu katika Imaan. Amma kwa ujumla hii yaqin ndio **Usul,** na amal nyingine zote zilobaki ni matawi tu ya Imaan katika dhati ya maana yake. Bwana Mtume S.A.W. amesema:-

"Hakika ndani ya mwili mna pande la damu likitengemaa hilo kimetengamaa kiwili wili kizima, na likiharibika hilo umeharibika mwili mzima, haitoshi kuwa ni moyo kitu hicho."

Kwa hadithi hii imeonyesha pia, kuwa Yaqin inaweza dhoofika kama vile kupata nguvu. Na ni kutokana nayo, ndiyo mazingatiwa ya ndani ya vitendo vyake Mtu. Bwana Luqman (Long man) alisema:

"Hakuna uwezo wa kufanya Amal yoyote ila ni kwa Yaqin, na hafanyi mja Amal yoyote ni kadiri ya Yaqin yake, wala haipungui Amal ya mtu hata ipungue yaqin yake mtu."

Na kutokana na ukweli huu kuna hadithi toka kwa Bwana Mtume S.A.W**.- "Yaqin ni Imaan yote"** yaani jumla ya Imaan yote nzima ni hiyo Yaqin kupata nguvu kwake. Na kama inavyotakiwa ni lazima iwe na nguvu, ni kwa kusikiliza Aya za Mnyezi Mungu, kwani Bwana Mtume S.A.W amesema :

"Kusikiliza Qur an kunarithisha Imaan".

Na pia kusikiliza labda… visa vyenye kujulisha Utukufu, Ukubwa, Upweke, Kibri, Ujabari na Ukamilifu wake Mnyezi Mungu, huko ni kuitia nguvu Yaqin. Inataka pia mja kupendelea sana kutazama ile **sanaa** ya Mnyezi Mungu iliyotapakaa kila mahali alipo mtu, maana hapana utapokuwepo isiwepo. Kutizama kwa jicho la kuzingatia. Na katika faida za Yaqin ni kupata mtu **Ishara** juu ya mambo mengi.

Qur an Fussilat 41:53.

سَنُرِيهِمْ ءَايَـٰتِنَا فِى ٱلْـَٔافَاقِ وَفِىٓ أَنفُسِهِمْ حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ
لَهُمْ أَنَّهُ ٱلْحَقُّ ۗ أَوَلَمْ يَكْفِ بِرَبِّكَ أَنَّهُۥ عَلَىٰ كُلِّ شَىْءٍ شَهِيدٌ ﴿٥٣﴾

"Tutawaonyesha (Ukweli wa) maneno yetu haya katika nchi za mbali na katika nafsi zao mpaka iwabainikie kwamba haya ni kweli."

Zaidi ya hayo inataka mara kwa mara Mja kuzidisha ile khofu yake na marejeo yake juu ya Mnyezi Mungu.

NGOME YA PILI

Ikhlaas:

Amesema Mnyezi Mungu; **Qur an Kahf 18:110**

فَمَن كَانَ يَرْجُوا۟ لِقَآءَ رَبِّهِۦ فَلْيَعْمَلْ عَمَلًا صَٰلِحًا
وَلَا يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهِۦٓ أَحَدًۢا ﴿١١٠﴾

"Anaependa kukutana na (Jaza ya) Mola wake na afanye vitendo vizuri wala asimshirikishe yoyote katika ibada ya Mola wake."

Huko ndiko kumtakasa Mnyezi Mungu bara-bbara na kila amali inazingatiwa na niya yake mtu na niya ni Moyoni ambako hakuna ajuaye illa Mnyezi Mungu. Bwana Mtume S.A.W. amesema:-

ا نما الاعمال با لنيات وانم لكل مرءمنو .....

"Kila amali itategemea niya ya Mja na kila mtu juu ya yale aliyonuiya…..".

Mmoja katika Mawalii maarufu **Karkhy** amesema:-

"Mwenye kufanya amal yoyote kwa ajili ya Thawabu, huwa amefanya biashara, na ikiwa ni kwa ajili ya kukhofu moto au kuwa na tamaa ya pepo, basi hukumu ya mtu huyo ni mtumwa, na mwenye kufanya Lillah huwa ni katika waungwana na hiyo ndio martaba ya juu yenye kila utukufu katika Ikhlaas."

Amesema Bwana Mtume S.A.W:-

"Ambaye ameacha dunia akiwa juu ya Ikhlaas Lillah, bila ya kumshirikisha Mnyezi Mungu na kutekeleza Sala na Zaka zake, basi atakuwa amefariki hali ya kuwa Mnyezi Mungu Radhi kabisa juu yake."

Ni juu ya mwanadamu kujilazimisha khassa kule kufanza amal zake njema kwa njia ya Ikhlaas ama siyo itakuwa ama imefanzwa kwa ajili ya kuonyesha mtu "Riya" Shirki (Walyadh Billah) Mnyezi Mungu atukinge nazo. Bwana Mtume S.A.W. alimwambia Bwana **Muadh bin Jabal:-**

"Tazama takasa dini yako itakutosha, amali chache wamefuzu wenye Ikhlaas kwani hao ndio taa za uongofu imewaepuka kila fitna ya Giza."

Watu watatu hawatapotea:

1. Moyo wa mtu aliyeamini.
2. Kutakasa amali yake Lillahi.
3. Mwenye kuleta maslaha kwa viongozi Waislamu.

Na yamefanzika majaribio kuona ya kwamba awezae kutekeleza amali zake kwa Ikhlaas akamcha Mnyezi Mungu, na kurayi amri za Qur-an na makatazo yake, na akala vya halali tupu kwa muda wa siku Arobaini basi (Moyo) hupata hikima toka moyoni mwake mpaka ulimi.

Amesema Bwana Mtume S.A.W:-

"Amefuzu ambae ameutakasa Moyo wake akaujaza kuamini kweli kweli kwa kupatikana Mnyezi Mungu aliyetukuka na akaamini Malaika wake, vitabu vyake, Mitume yake, siku ya mwisho na akatenda amali njema, ambaye ameutakasa moyo wake kwa Imaan, akaujaalia moyo ni wenye kunyenyekea na ulimi wake ni wenye kukubali

na nafsi yake ni yenye kutulia kwa Mnyezi Mungu juu ya kila masaibu yampatayo akaacha kusema kila ambalo linamghadhibisha Mola wake asikasirike wala kukata tamaa, na akawa na tabia iliyonyooka yaani akijitukuza kwa tabia njema, akaangalia sikio lake ni lenye kusikiza ya kheri matupu, na macho yake ni yenye kuangalia mema matupu.

Pia amesema Bwana Mtume S.A.W :-

"Hakika si vingine Sala ni yenye msaada sana kwa kumpwekesha mnyezi Mungu."

Ikhlaas imeendelea, ni kitu ndani ya moyo kinachohitaji nia njema kule kutekelezwa kwake, na kupatikana amali kwa njia ya Mnyezi Mungu pekee yaani Lillahi Taala.

Amesema Ibn Abbas (R.A) Ammi yake Bwana Mtume S.A.W. (huyu riwaya yake ni yenye kutegemewa sana kwa sababu yeye mwenyewe alikuwepo zama hizo hizo Qur an ikishushwa na alikuwa na kila fursa nzuri ya kufahamu vyema kila kitu)

"Kuacha kufanya amali kwa ajili ya (Kuonyesha) watu,(Riya) na kufanza amali kwa ajili ya watu (Wakuone) hiyo ni shirki, na Ikhlaas ni zama Mnyezi Mungu atapokuafu kutokana na mawili hayo."

Aliulizwa Bwana Mtume S.A.W:- "Nini Imaan?" Akasema, **"Imaan ni Ikhlaas"** na hakika si vingine ni jambo la kumlazimu mtu kutekeleza amali zake zote Lillahi Taala, kwa kila hali. Kwa sababu Mnyezi Mungu husamehe mabaya yote ghairi ya yale ya kumshirikisha.

Pia juu ya Ikhlaas amesema Mnyezi Mungu: **Bayyina 98:5.**

وَمَآ أُمِرُوٓاْ إِلَّا لِيَعۡبُدُواْ ٱللَّهَ

"Na sikuamrishwa ila kumwabudu Mnyezi Mungu,"

Kadhalika ametuambia tena:

"….Illa Ibadaka Minhumul Mukhlasina…"

"Isipokua wale waja wako waliosafika kweli kweli…."

Yaani Iblis (Alayhil Laana) atawaingia watu wa kila aina, bali wale watekelezao amali zao Lillahi ni vigumu, na hawezi kabisa hata kuwakurubia.

NGOME YA TATU

Kutekeleza Faradhi:

Qur an 85:11.

إِنَّ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ لَهُمۡ جَنَّٰتٞ تَجۡرِي
مِن تَحۡتِهَا ٱلۡأَنۡهَٰرُۚ ذَٰلِكَ ٱلۡفَوۡزُ ٱلۡكَبِيرُ ١١

"Hakika ya wale walioamini na wakatekeleza amali njema basi jaza yao ni hiyo bustani ya pepo ipitayo chini yake mito (Yaani mito ya pombe (mvinyo) asali, maziwa na maji yaliyo na ladha ya ajabu kwa wanywao), huko ndiko kufuzu kuliko kuwa kukubwa."

Aya hii ni yenye kushadidia hadithi ya Bwana Mtume S.A.W. tulokwisha ipitia, juu ya kutekeleza amali zote ambazo zimefaridhiwa, baada ya kumjua Mnyezi Mungu kwa yaqin kabisa. Hakika si vingine utekelezaji wa faradhi ni jambo lenye kumkaribisha mtu na Mola wake haraka kabisa. Hapa hatuna budi kubainisha mfano wake yeye Bwana Mtume S.A.W. mwenyewe ambae juu ya kupewa darka na Mnyezi Mungu kuwa hana dhambi (Impeccable) kwa kauli ya:

Qur an Fat hi 48 : 2.

لِّيَغۡفِرَ لَكَ ٱللَّهُ مَا تَقَدَّمَ مِن ذَنۢبِكَ وَمَا تَأَخَّرَ
وَيُتِمَّ نِعۡمَتَهُۥ عَلَيۡكَ وَيَهۡدِيَكَ صِرَٰطٗا مُّسۡتَقِيمٗا ٢

"Amekufutia (Amekusamehe) Mwenyezi Mungu, yaliyotangulia katika dhambizako, na zitakazo kuja."

Lakini na papo, hakuacha kuwa mwenye kusimama usiku kusali mpaka ikamshitaki miguu yake (kwa kuvimba) kama walivyomsifu washairi mfano wa **Imam Busir** na kama alivyomuelezea Mnyezi Mungu mwenyewe katika **Hadithil Qudsi** ambazo Bwana Mtume S.A.W. alizipokea toka kwa Mnyezi Mungu Mtukufu, ni ile isemayo:-

"Hakukurubia mbele zangu mja na kitu kinachonip endezesha mno zaidi kuliko yale niliyomfaraidhia juu yake kuyatekeleza, na wala hataacha mja wangu kunikaribia kwa Sunna zangu, mpaka awe miongoni mwa niwapendao na zama nikimpenda basi huwa mimi ni sikio lake ambalo husikilia kwalo, na jicho lake ambalo kwalo huonea na mkono wake ambao anaufanyia kazi nao, na mguu wake ambao anautembelea nao, na lau anaomba humpa, na ajikingapo na kitu humkinga na hazingizingi juu ya jambo lolote ila nami huzingazinga juu yake, na hawi mwenye kuchukia huko, hata ikiwa ni juu ya haki kama vile kufa"

Kutekeleza faraidhi ni asili ya amri yake Mnyezi Mungu, amma sunna zenye kufwata, na ni muhimu zinapotoka zote mbili kwa wakati mmoja, kutanguliza asili . Tafauti na inapotoka faraidhi tupu kwa wakati mmoja ambapo yoyote itangulizwayo hufaa tu.

Katika Wajihi huu imekokotezwa mno kujinadhifisha nje na ndani (Dhahir na Batin) kwani mwenye kukamilika na nadhifa hiyo basi roho yake ruhani, na lau kiwiliwili chake yu aonekana ni mtu. Katika kufikia hali hii mwanadamu huwa amezidi Malaika kwa daraja, kwa sababu, tofauti kubwa katikati hakuna ila ni **matamanio,** ambayo Malaika hakupewa asili. Lakini kama ni akili wanayo wote na kadhalika. Hii ni sawa na mfano wa Seyyidna Idris A.S jinsi Malaika walivyoweza kumuhusudu kwa Ibada yake mpaka kufika kupaa. Kwa kujinadhifisha, Bwana Mtume S,A.W. amesema:-

"Hakika ya Mnyezi Mungu aliyetukuka,
ni mwenye kupenda unadhifu (kwa sababu
Yeye mwenyewe ni nadhifu) basi jinadhifisheni".

Pia amesema:

"Uislam ni nadhifu, basi jinadhifisheni,
kwani haingii mtu peponi illa nadhifu"

Unadhifu huu sio wa kuoga na kuvaa kanzu peke yake laa, makusudiwa ni unadhifu wa nguo, mwili na roho pia. Hakika ya unadhifu wa ndani haupatikani ila kwa kutakasa nafsi na machafu yote, kwani kama tunavyopaswa kuelewa ya kuwa nafsi daima huamrisha maovu ni lazima tuelewe ya kuwa kutakaswa mpaka kufikia ile hali aliyotwambia Mola. Na zaidi ya kutekeleza faraidh ni kuamrisha mema na kukanya mabaya kuamini faradhi ya kutoshelezana hiyo Mnyezi Mungu ametuambia: **Qur an Ahqaf 46:13.**

إِنَّ ٱلَّذِينَ قَالُواْ رَبُّنَا ٱللَّهُ ثُمَّ ٱسْتَقَٰمُواْ فَلَا خَوْفٌ
عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿١٣﴾

"Hakika ya wale waliosema Mola wetu ni Mwenyezi Mungu kisha wakasimama kufanza Ibada hawatakuwa Na khofu (siku ya kufa kwao wala baadaye) wala Hawatahuzunika".

Pia huko kusimama kufanya Twaa, maana yake ni kukubali kwa moyo mmoja na kufanya Twaa kwa kila hali pamoja na kuwa na **Ihsaan** yaani kule kumwabudu Mnyezi Mungu kama unaemuona, ukijua ikiwa humuoni basi yeye anakuona.

Mwisho tunasema juu yake kwa kauli ya Mnyezi Mungu:

Qur an Hadyd 57:16.

۞ أَلَمْ يَأْنِ لِلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ أَن تَخْشَعَ قُلُوبُهُمْ لِذِكْرِ ٱللَّهِ وَمَا نَزَلَ مِنَ ٱلْحَقِّ
وَلَا يَكُونُواْ كَٱلَّذِينَ أُوتُواْ ٱلْكِتَٰبَ مِن قَبْلُ فَطَالَ عَلَيْهِمُ ٱلْأَمَدُ فَقَسَتْ
قُلُوبُهُمْ ۖ وَكَثِيرٌ مِّنْهُمْ فَٰسِقُونَ ﴿١٦﴾

"Je, wakati haujifika tu kwa wale walioamini kwamba nyoyo zao zinyenyekee kwa kumkumbuka Mnyezi Mungu na kwa mambo ya haki yalioteremka wala wasiwe kama wale waliopewa kitabu zamani (Mayahudi na Manasara) na muda wao (Wa kuondokewa na Mitume) ukawa mrefu, kwa hiyo sasa nyoyo zao zikawa ngumu na wengi wao wakawa waasi".

NGOME YA NNE.

Kuacha yaliyoharamishwa:

Imaan maana yake, ni kuacha yote ambayo Mnyezi Mungu ameyaharamisha, baada ya kumjua baraab-bara Mnyezi Mungu mwenyewe, kumtambua kwake inakuwa ni hivyo. Kumtambua Mnyezi Mungu ni Ibada, na kujiepusha na yale aliyoyakataza ni moja ya Ibada kubwa mno, kwa sababu sio rahisi kufanza hivyo.

Amesema Bwana Mtume S.A.W:

"Hafikii mmoja wenu darja ya uchaji Mungu mpaka awache lisilodhuru kwa hadhar ya kuchelea lenye kudhuru"

Hadithi hii inaoyesha ya kwamba kabla ya kupatwa na mitihani inafaa mtu kukwepa yote ambayo yanaweza kuleta mithani. Ndo kusema jambo lolote na falau halina lawama si uzuri kulidharau, kwani kwa mazowea ya ubinadamu ukiudharau mwiba matokeo huwa ni kupata bude.

Imesemekana ya kuwa kwa asiye ijuwa shari, basi huwingia bila kujijua. Muharramaat ni mambo ya shari haitoshi kukaa tu bila kuyajua ni yapi ikamaanisha ndiyo umesalimika nayo.

Amesema Bwana Mtume S.A.W:-

"Mnyezi Mungu ni mzuri, yu wapenda mazuri".

Na ubaya wa yote hayo umo ndani ya ukweli kwamba haitimu amali yoyote illa kwa kujitingisha, na kutingishika viungo hutegemea nguvu ambayo hupatikana kwa sababu ya chakula basi kilicho muhimu ni hicho chakula. Ikiwa ni kilichopatikana kwa njia ya halali amali yoyote utayoifanya itakuwa ni ya halali (Amali yoyote hiyo tabaan ni katika zilozoamrishwa kufanzwa) na chakula kupatikana kwake, lau ni njia ya haramu au shubha, basi amali yoyote ile utakayofanya itakuwa ni ya kikhabithi tu.

Muallifa wa kitabu **"Zubad".** Amesema :

"Na Twaa, kutokana na chakula cha haramu, ni kama kujalia msingi juu ya mavumbi".

Amesema Bwana Mtume S.A.W:

"Mwenye kuingia kwenye shub-ha, basi ameingia kwenye haramu".

Hadithi inafahamisha juu ya mambo ambayo haijatoa faswihi kamili juu ya kuwa kwake halali au haramu. Yaani yanakuwa mashkuk kidogo katika kule kuamulika kwake, basi hayo pia pindi mtu akiingia ndani yake huwa ameishaingia katika haramu. Yote hayo ni katika kuchunga tu mtu asiwe atatekeleza Ibada yake kutokana na kipato cha haramu. Fakaifa ambao riziki zao ni kutokana na pato la dhulma, ribaa, ulevi na makamari, au uasherati lini Ya-Rab Twaa yake itakuwa imesimama sawa sawa?.

Watu ni wa aina tatu:

1. Amma atakuwa mtu ambae unamjua, si mgeni kabisa mbele yako kwa majambo ya kheri au Sulhu, huyo una rukhsa kula pindi akupapo kitu chochote cha kula.
2. Amma mtu atakuwa hajulikani mbele zako kwa mambo ya kheri humjui kabisa wala kwa mambo ya shari, basi pindi ikiwa ndo kupokea hidaya yoyote toka kwake inatakiwa haraka kuuliza rafiki, la ikiwa italeta maudhi moyoni mwake basi kunyamaa ni awla. Kwani lau itakuwa unatafuta njia za usalama wako lakini pia maudhi Bwana Mtume S.A.W. hakuyapendelea.

   "Wala usimkabili Mwislam mwezio kwa jambo lolote la kumchukiza"

3 Amma mtu atakuwa ni maarufu kwako kuwa dhaalim huyo, kwa atakacho kuhidia inafaa kutokipokea, na lau amesema Bwana Mtume S.A.W:-

"Hawi ni mwenye kuamini kikweli, ambaye anarudisha hidaya."

Kwa sababu hidaya huwa ni yenye kutoka kwa Mnyezi Mungu (Illal – Laim: yaani hidaya mbaya, basi utapaswa kuiainisha hidaya yenyewe) na mwenye kuirudisha huwa amemrudishia Mnyezi Mungu

NGOME YA TANO.

Kutekeleza wajibati:

Wajibu kama ilivyo maaruf, ni jambo lililokuwa lazima. Na ni sawa katika kulitekeleza kwake mtu hupata thawabu na akiliacha hupata dhambi. Amma wajibu wa kwanza kwa Muislam ni kumjua Mnyezi Mungu kwa yaqin kabisa.

Kwa jumla, ni lazima kuitakidi ya kuwa hakika ya Mnyezi Mungu Mtukufu amesifika kwa kila sifa kamilifu, na ameepukika na kila sifa pungufu kwake kadhalika ikubali akili Mnyezi Mungu ni mwenye kupatikana, na ni muhali kukosekana katika ulimwengu. Isitoshe, **Yeye** ni Watangu na Watangu, si ambae amezuka tu, tena ni mwenye kubaki, kinyume cha kuwapo siku moja Atakufa – Ataondoka.

Mnyezi Mungu hakuna wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa **Yeye** mwenye uhai wa milele na Mwendeshaji wa mambo yote. Ambae hakuna Mola apaswae kuabudiwa kwa kweli ila **Yeye** ambae **Yu hai** daima amesimama hafi.

Kila nafsi ni yenye kufa na kuhiliki. Amesimama Mnyezi Mungu kwa nafsi yake, si ambae amechegama au kujishikiza na chochote chenye kuondoka. Na ni Mmoja peke yake hana mshirika wala Idadi.

"Hakika Mola wenu ni Mmoja peke yake."

Ni wajibu kwake tu kustahili Uwezo na ni kinyume kushindwa na chochote kile. Tena ni Mwenye kutaka juu ya kila jambo pindi linapotuka, si ambae analazimishwa kwani si vingine ila ni kwa ……

كن فيكون "Kuwa " - "Inakuwa"

Hakika amri yake zama anapotaka kitu chochote kile kutuka ni kusema (Kukiambia) "kuwa" na huwa mara hiyo hiyo bila kinyume chochote. Yeye ni mwenye Ilimu si kwamba alijifundisha hapo kwanza, ambapo itamaanisha alikuwa mjiga kama ilivyo kwetu sisi viumbe. Mnyezi Mungu ni mwenye Uhai wa milele **hafi.** Anasikia lau si kwa viungo, kwani hafanani na kitu chochote, haitoingia akilini kuwa yeye ni kiziwi kama isivyo ingia akilini kuwa bubu na kipofu wakati yeye amesifika na ukamilifu wa sifa za kuwa mwenye kuona na kusema

bila kuwa maneno yake ni yenye kupandishwa au kuwa ni harfu na lafdhi kama yetu, ndio yasikike. Mfano mdogo kwetu sisi ni juu ya ndoto, ambapo inaweza kutoa dalili ndogo kabisa kuthibitisha kutokuwepo lazima kupandanisha maneno kwa herfu na lafdhi ili isikike, wakati mtu anajiona anapiga makelele sana lakini hayamsikizi yeyote kati ya walo macho, karibu ya kitanda chake.

Mnyezi Mungu ni **Muweza** hana lenye kumshinda ni kutaka, si mtenza nguvu kwa lolote, **Mjuzi** si jahili, **Yuhai**, hategemewi **kufa** mwenye kusifika, kuona na kusema, si kiziwi, kipofu au bubu hata kidogo na ni muhali asingekuwa mkamilifu wa sifa. Ni mamoja kwa Mnyezi Mungu kufanya kila kinachomkinika au kuacha kufanya. Kwa kiasi tu ni yenye kutosha kwa ufahamisho wa kutekeleza wajibati.

Muumini anajishughulisha kuyajua yote yale aliyowajibishwa juu yake. Kwani tumekwisha bainishiwa kuwa ni wajibu wa kila Muislam Mume na mke kutafuta Ilimu, na kufahamu kuwa mjinga ni adui wa Mnyezi Mungu.

NGOME YA SITA.

Kutekeleza Sunna:

Kama inavyoeleweka kuwa Sunna ni jamii ya vitendo vyote alivyovifanya Bwana Mtume S.A.W. imekuwa ni fungu katika dhati ya maana ya Imaan, Mnyezi Mungu amesema…**Qur an Hashr 59:7.**

وَمَآ ءَاتَىٰكُمُ ٱلرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَىٰكُمْ عَنْهُ فَٱنتَهُوا۟ ۚ

"Na anachokupeni Mtume, basi pokeeni, na anachokukatazeni jiepusheni nacho".

Aya hii ni madhubuti kabisa katika kuonyesha ya kuwa hakuna shaka yoyote muumini atazitekeleza tu Sunna za Bwana Mtume S.A.W. akiwa pia na mategemeo makubwa ya kufutiwa dhambi zake na angaa hajaleta Stighfar.

Vitendo alivyofanya Bwana Mtume S.A.W. vyote vimethibitiwa madhubuti havipotei na Mnyezi Mungu ametuambia.

Amma katika vitendo vya Bwana Mtume S.A.W. vilivyo vikubwa ni kupiga mswaki, Ndoa, Sala za Rawatibu yaani zile za rakaa mbili, kufuata jeneza, kuwasaidia waliofiwa na waume zao na hawakuolewa. Kuwatokea watu kwa wajihi mkunjufu wenye bashasha na kadhalika.

Amma katika kila alichokifanya Bwana Mtume kilikuwa na mafunzo mengi ndani yake na mvuto wa raha kubwa mno kwa mtu mwenye akili. Na falau vitendo vyake ni vyenye kushikamana sana kwa kila njia, na **Qur an Tukufu,** lakini Wallahi kitendo chake cha kukaa na maskini na watu dhaifu na kuzungumza nao mazungumzo ya furaha, ya busara na kupooza moyo, hicho ni kitendo kisichokua na mfano. Hicho ni kitendo kilichokua kitukufu sana, na chenye mvuto wa ajabu na chenye miujiza na siri kubwa ndani yake, ukizingatia jinsi yeye alivyokuwa kwa jumla. Kwa kifupi akiwa yeye kama kiongozi wa ulimwengu mzima, mimi na wewe labda tusingemtegemea hata kwa dakika moja kumkuta katika au miongoni mwa kundi la watu wa aina hiyo. Watu ambao ni duni wachafu, hawana pesa wala nguo za maana, watu ambao shida haziwaishii kila dakika na watu ambao wana chungu ya athari za kasoro na mwisho wa yote ni watu ambao hatungetegemea kumpata kwao Bwana Mtukufu kama yeye hata siku moja, lau tungekuwa tunamtafuta. Lakini kinyume ya mambo eti yeye ndio alikuwa baraza yao ya kila siku. Sidhani

kama ulimwengu wetu wa leo umethamini sana kitendo hiki. Na wale wachache waliochukua tabia hii wamefikia kipeo cha kupendeka na kila mtu. Mfano mdogo tu ni wa Khalifa Harun Rashid, Abraham Lincolin Rooservet nk.

katika vitendo vya Bwana Mtume S.A.W. upole pia ulitia fora la mvuto mkubwa. Hekaya ya Mnyesheleza bustani ni moja yenye nguvu kuifahamu zama Bwana Mtume S.A.W alipojitolea kutafuta kibarua chochote ili apate angalau kokwa mbili za tende kwa wajukuu zake Seyyidna Hassan na Husseyn. Akakubali kumsaidia Bedui huyo kuchota maji toka kisimani kumwagia bustani kwa ujira wa tende moja kila debe. Baada ya kufaulu kuchota madebe mawili matatu kamba ilikatika na debe likatumbukia kisimani. Bedui kwa hasira ya kuharibiwa kazi yake alimpiga Bwana Mtume S.A.W. kibao kizito mno usoni, pamoja na kumtusi na kumlaani, lakini lau uso wake ulipiga wekundu kwa damu yeye mwenyewe hakuonyesha kuwa na hasira wala chuki, badala yake Bedui alimuona ni mwenye bashasha kama ile aliyokuja nayo na kuwa nayo zama akifanya kazi yake ingawa alimlipa ujira wake tende chache na akazipokea kwa uso mkunjufu na ahsante ndo akaenda zake lakini Bedui hakuacha kuwaza juu yake kuwa ni mtu wa aina gani yule, isije ikawa ndo yule anaemsikia Makureish wakimsema kuwa ni Mtume wa Waislamu.

Alipotia na kutoa na kuhakikisha kuwa lazima ni huyo alifikiria uamuzi wa kulikata lile ganja lake lilompiga Bwana Mtume S.A.W. na akamfwata akiwa ameushikilia vile vile unavuja damu mpaka kwa wajukuu zake ambako alimkuta anacheza nao, wote wawili wamempandia mgongoni kwake kama farasi, nae anawaendesha. Bwana Mtume S.A.W. aliposikia hadithi ya Bedui, vile alivyojifanza alikishika kile kiganja akaomba dua kikawa kama hakijakatwa na bila maumivu, pale pale Bedui ilimwingia **Imaan** akatoa shahada.

Tukidadisi juu ya kisa hiki tutaona upole tu umekuwa ni waadh wa kutosha, kumfunza mtu kumtambua Mnyezi Mungu na kutuhakikishia kuwa tabia yenye manufaa makubwa mno katika dini yake Mnyezi Mungu.

NGOME YA SABA.

Adabu:

Katika ukamilifu wa maana ya Imaan adabu imesadifika ngome ya mwisho kama ilivyokuwa Qudra kwa upande ule mwingine.
Bwana Mtume S.A.W. amesema katika hadithi iliyopokelewa na Bwana **Dylamy:**

"Wafunzeni adabu watoto wenu juu ya mambno matatu:-

1. Kumpenda Mtume wenu.

2. Kupenda watu wa nyumbani kwake na

3. Kusoma Qur an. Basi kwa hakika mwenye kuhifadhi (kwa moyo) yu katika kivuli chake Mnyezi Mungu siku ambayo hakuna kivuli ila kivuli chake Mnyezi Mungu pamoja na Mitume yake na watu wema".

Na adabu imewekwa ndani ya kila jambo alifanyalo mtu, kuanzia kula, kulala kusoma, kukutana na watu, kwenda haja ndogo au kubwa, ikiwa ni chooni au kwenye mawanda na katika mambo yote hayo inahitajiwa hali ya kuwa ni lazima juu ya mtu (aliyeamini) kujifunza ayajue bara-bara.

Amma katika adabu kwa sababu, si jambo geni mno katika maisha yetu ya kila siku, tumechukua mfano mzuri mno ka tika hadithi ya Bwana Mtume SAW:-

"Nimiletwa kwenu nyinyi ili kutimiza tabiya nzuri kwani Lau ningechaguzwa kwa jambo lolote lile kuzidi, nisingechagua jingine lisilokuwa tabia njema kwani kila cha fadhila kikushukiacho (na kukutoka) huisha tu, isipokuwa sifa nzuri, kwani hizi hubaki nawe" (Na lau umesha kufa, lakini waliohai lazima watazizungumza).

Katika hadithi nyingine Bwana Mtume S.A.W. ametuhimiza tujipambe nazo hizo tabiya njema kwa kutwambia:

"Mtu hua ni hadithi baada yake, basi kuwa hadithi iliyo nzuri kwa watakayoipiga"

Ukamilifu wa mambo hayo yote ndiyo dhati ya maana ya **Imaan** ambayo kama utaichunguza vizuri utaona bila shaka yoyote ni kamili. Kwa hivyo bila kusita tutasema ya kuwa: **Dini ni Imaan**. Na lau itapungua moja katika ngome zake au nguzo zake basi Uislamu au Dini yake mtu si kamili na ni vigumu kuitwa Mwislam.

Hadithi zote hizo ni zenye kuweka kikazo kuwa amependelea Bwana Mtume SAW juu yetu kuwa na tabia nzuri nzuri katika maisha yetu ya hapa duniani, na hatuwezi kuipata tabia nzuri popote pale kuliko alipotuagizia yeye mwenyewe kwa wasia:-

"Allahumma Salli Wasallim Allayh."

WABILLAHIT TAWFEEQ.